# OFISI YA RAISI- TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
# HALMASHAURI YA MJI BARIADI
# SHULE YA SEKONDARI KIDINDA

**S.L.P 208- BARIADI**

***kidindasecondary@yahoo.com***

**SIMU: 0679 609 638 / 0787 345 379**


**Kumb. Na: KSS/02021/001** **18/12/2020**

**Jina la Mwanafunzi**………………………………………………………………………
**S.L.P**………………………………………………………………………………………

## Yah: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKODNARI KIDINDA MWAKA 2021

### 1. UTANGULIZI

Nina furaha kukuarifu kwamba **UMECHAGULIWA** kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekodnari Kidinda mwaka **2021**. Shule ya sekondari Kidinda ipo umbali wa km 2 Magharibi mwa Halmashauri ya Mji Bariadi, pembeno ya barabara iendayo Mwanza kupitia Ngulyati mbele kidogo ya Mnada wa Ng'ombe wa Kidinda – Bariadi.

Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe **11/01/2021**. Unatakiwa kuripoti shule kuanzia tarehe **11/01/2021** kwa ajili ya usajili na maelekezo ya taratibu za shule na mwisho wa kuripoti ni tarehe **18/01/2020** (ndani ya siku saba) ambapo taarifa itatolewa kwa wasioripoti.

### 2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

#### 2.1 Sare za shule

A. Sare za shule kwa **WAVULANA** ni shati mbili (2) nyeupe za mikono mifupi, viatu vyeusi vya kufunga kamba vyenye visigino vifupi (**buti/yeboyebo haviruhusiwi**), soksi rangi ya kijivu jozi mbili, suruali mbili (moja rangi ya damu ya mzee na nyingine rangi ya buluu-nyeusi (dark blue) na zisiwe za kubana (**model**), sweta la kijani, tai mbili moja ya rangi ya damu yam zee na nyingine rangi ya bluu-nyeusi (Dark blue) na mkanda mweui wa wastani na usio na chata au michoro yoyote ile.

B. Sare kwa **WASICHANA** ni ni shati mbili (2) nyeupe za mikono mifupi, viatu vyeusi vya juma na roza au vya kufunga kamba vyenye visigino vifupi (**buti/yeboyebo haviruhusiwi**), soksi rangi nyeupe jozi mbili (2), sketi mbili **ndefu za kufunika soksi aina ya rinda box** moja ya rangi ya damu yam zee na ya pili ya rangi ya buluu-nyeusi (Dark blue), sweta

la kijani, tai mbili moja ya rangi ya damu yam zee na nyingine rangi ya bluu-nyeusi (Dark blue).

C. Rangi ya **Hijab** ifanane na sare za shule

D. Sare ya michezo ya shule kwa **WAVULANA** ni tracksuit ya bluu, raba jozi moja, soksi ndefu za kijivu na fulana ya buluu

   Kwa **WASICHANA:** tracksuit ya bluu, raba nyeupe, soksi nyeupe na fulana rangi ya buluu.

### 2.2 Mahitaji ya Kitaaluma

i. Daftari kubwa zenye jalada gumu (**COUNTER BOOKS**) kumi (10)
ii. Kalamu za buluu au nyeusi na penseli
iii. Mkebe wenye vifaa vya hisabati (Mathematical set)
iv. Kamusi ya kiingerza kwa kiingeleza (English – English dictionary)
v. Mfuko/begi la kubebea vifaa vya kitaaluma (daftari, kalamu n.k)

## 3. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaja 1995. Aidha inaingia sera ya elimu ya mwaka 2014, nyaraka na miongozo yote inayotolewa na ofisi ya raisi, tawala za mikoa na serikali ya mitaa yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini.

### 3.1 Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wanafunzi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima
iii. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa .
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya hiyo wakati wote wa uwanafunzi wako shuleni.
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unaotakiwa kufanya hivyo ni lazima
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote unapotakiwa
ix. Kutunza mali zote za umma.

### 3.2 Makosa yafuatayo yanaweza kukusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule.

i. Wizi
ii. Uasherati na ushoga
iii. Ubakaji
iv. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika

v. Kupigana au kupiga
vi. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
vii. Kudharau bendera na wimbo wa taifa
viii. Kuwa mjamzito au kupata mimba
ix. Kuoa au kuolewa
x. Kugoma, kuchochea, kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
xi. Kukataa adhabu kwa makusudi
xii. Kuwa na simu ya mkononi.

**4. MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI**

i. "Medical Examination Form" ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.
ii. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

***Tafadhari soma kwa makini maelezo/ maagizo yote na kuyatekeleza kikamilifu***

# KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI KIDNDA

……………………………………

**MHINGA B. MALONGETA**
**MKUU WA SHULE.**

# OFISI YA RAISI- TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**HALMASHAURI YA MJI BARIADI**
**SHULE YA SEKONDARI KIDINDA**
**S.L.P 208- BARIADI**
**kidindasecondary@yahoo.com**
**SIMU: 0679 609 638 / 0787 345 379**

## ***Kiambatisho A*: FOMU YA MAELEKEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI NA MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI**

Anwani ya Mwanafunzi:
S.L.P......................
BARIADI.

MKUU WA SHULE,
SHULE YA SEKONDARI KIDINDA,
S.L.P 208- BARIADI.

Mimi...............................................................ambaye ni mwanafunzi niliyechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza 2021 katika shule ya sekondari Kidinda, nakubali kujiunga na shule hii. Naahidi kuwa nitakuwa mwanafunzi mtiifu, mwadilifu na kuwa nitafuata sheria na taratibu zote za shule. Nitatunza mali zote za umma zilizopo shuleni na nitasoma kwa bidii na uwezo wangu wote, nitashirikiana kikamilifu na wanafunzi wenzangu katika kazi zote za shuleni na darasani, nje au michezo. Nitaishi kwa amani  na kujiheshimu katika jumuiya ya shule na jumuiya inayoizunguka shule. Pia, naapa kuwa sitashirki katika migomo, fujo yoyote na sitatenda kosa lolote la jinai na ikitokea hivyo hatua kali za kinidhamu na za  kisheria zichukuliwe dhidi yangu ikiwemo kufukuzwa shule mara moja

| ................................ | ........................ | .................................... |
|---|---|---|
| SAHIHI YA MWANAFUNZI | TAREHE | Mbele ya Makamu Mkuu wa Shule |

## ***Kiambatisho B*: FOMU YA MZAZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA MAELEKEZO MENGINE YATAKAYOTOLEWA NA SHULE**

**PICHA YA MWANAFUNZI**

Awani ya mzazi
S.L.P ..............................
BARIADI.
Simu...................................(NI MUHIMU)

Mimi.......................................................mzazi/mlezi wa..............................
Ambaye ni mwanafunzi wa shule ya sekondari kidinda naapa kuwa:

a) Mtoto wangu atafika shuleni na vifaa vyote vilivyoagizwa na shule katika fomu hii.
b) Nitashirikiana na jumuiya ya shule kumsisitiza mwanangu kufuata sheria zote za shule.
c) Mtoto wangu awapo nyumbani nitampatia muda na mazingira mazuri ya kujifunzia, kufanya mazoezi aliyopatiwa na walimu wake (home work) na nitamuelekeza pale nitakapoweza.
d) Sitakubali mwanangu kutohudhuria shuleni siku za masomo bila taarfa ya maandishi kwa uongozi wa shule. Nitaomba ruhusa kwa walimu endapo kuna tatizo lolote.
e) Niko tayari kuchukuliwa hatua  kali za kisheria pindi nitakapo kiuka kiapo hiki.

| ................................ | ........................ | .................................... |
|---|---|---|
| **SAHIHI YA MWANAFUNZI** | **TAREHE** | **Mbele ya Makamu Mkuu wa Shule** |

**THE PRESIDENT OFFICE, REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

# BARIADI TOWN COUCIL

Kidinda Secondary School,
P.O.BOX 208,
**BARIADI.**

**To Medical Officer,**

…………………………………

…………………………………

**BARIADI.**

**RE: FORM FOR MEDICAL EXAMINATION**

Please examine the above-mentioned Boy/Girl as to his/her fitness for studies at the school (This form be completed by Government medical officer)

**Student's Full Name**:……………………………………………………**Age**……….**Sex**………

| | |
|---|---|
| Blood test | ………………………………………………………… …… |
| Stool and urine examination | ………………………………………………………………… |
| Asthma | ………………………………………………………………… |
| Eye/ sight disorder | ………………………………………………………………… |
| Ear disorder | ………………………………………………………………… |
| Mental condition | ………………………………………………………………… |
| Anemia | ………………………………………………………………… |
| Chest (TB) | ……………………………………………………… ………… |
| Operation | ………………………………………………………………… |
| Serious accidents | ………………………………………………………………… |
| Any other infectious diseases | ………………………………………………………………… |
| Pregnancy | ………………………………………………………………… |

**ADDITIONAL INFORMATION** (e.g. Physical defects or impairments) infections chronic of family disease etc

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

I ***certify*** that above is fit to pursue studies as indicated above

**Signature:** ……………………………………………………

**Designation:** ……………………………………………………

**Station:** ……………………………………………………

**Date:** ……………………………………………………